NTIMA, NYAKI AND MUNICIPALITY CLUSTER EVALUATION - 2016

# KISWAHILI (FASIHI)

Karatasi - 102/3

**Julai / Agosti - 2016**

## MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

**1. USHAIRI**

**a)**

i) kuwa wazalendo / kuipenda nchi yako.
ii) kuwa na umoja / kuacha ukabila.
iii) kulinda demokrasia
iv) kuwa na mgao sawa wa raslimali
v) kuacha tamaa
vi) kukomesha uhalifu
vii) kuacha maringo
viii) kuacha ubinafsi / kusaidiana.
ix) kutii katiba

***za kwanza 4 × 1 = 4***

**b)**

i) Msemo - Nipe masikioni - Nipe sikio.
ii) Jazanda / istiari - kawa mpinde.
iii) Takriri - taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.
iv) Tashbihi - kama mtu mswahili.
v) Utohozi - Demokrasia, bajeti

***ya kwanza 1 × 2 = 2***

**c)** Ukaraguni - Vina vya kati na vya mwisho vinabadilikabadilika kutoka ubeti hadi mwigine.

***1 × 1 = 1***

**d)** Mwananchi / raia / mzalendo / mkereketwa

***1 × 2 = 2***

**e)** Himiza / nasihi / shawishi.

***1 × 2 = 2***

**f)**

i) Kubananga / kufinyanga / kuboronga sarufi - Uongozi tushiriki - tushiriki uongozi, changu naweza tetea - naweza tetea changu.
Umuhimu - Kuleta urari wa vina
ii) Utohozi - Demokrasia
Umuhimu - Kuleta urari wa mizani
- Kulipa upekee
iii) Inkisari - Pasi - pasipo
- Wachotaka - Wachotaka.
Umuhimu - Kuleta urari wa mizani

***za kwanza 2 × 2 = 4***

***aina - 1***

***umuhimu - 1***

**g)** Naanza kwa kueleza uzalendo kwamba tuipende nchi yetu / matendo yetu yaonyeshe kuwa tunailinda nchi yetu / tabia ya kila mtu ionyeshe msimamo / nchi haikamiliki bila kuwa na mtendo mema.

***4 × 1 = 4***

h) hongo - rushwa / mlunguva / chai / kadhongo.

***1 × 1 = 1***

**2.a)**

i) a) Msemaji - Madhubuti
b) Msemewa - Amani
c) Wamo kibandani mwa Amani
d) Wanazungumza namna ya kuleta mabadiliko Tomoko.

***4 × 1 = 4***

ii) Kuchanganya ndimi - Revolution.

***1 × 2 = 2***

**b)**

i) Kuna ufisadi k.m. Nasaba Bora kuhonga ili Madhubuti apate kazi.
ii) Kuna mauaji k.m. Chichiri Hamadi.
iii) Unyakuzi wa ardhi k.m. shamba la akina Imani
iv) Kuna udikteta k.m watu kulazimishwa kuhudhuria mikutano.
v) Kutowajibika kwa wafanyakazi k.m wauguzi, majisifu n.k.
vi) Ajira za watoto wadogo k.m . Dj kwa Bw. Maozi.
vii) Visingizio km. Amani na Imani kusingiziwa kifo cha kitoto Uhuru.
viii) Wizi km. wizi wa miswada.
ix) Ufadhili wa watoto maskini kutumiwa na matajiri k.m Fao.
x) Undandanyifu katika mitihani k.m Fao kufanyiwa mtihani.
xi) Uzinzi k.m Nasaba Bora na Lowela.
xii) Mashujaa kutelekezwa k.m Matuko, Chwechwe n.k.

***za kwanza 7 × 2 = 14***

**3.a) Sadfa** - kutokea kwa mambo mawili au zaidi bila kupangwa wala kutarajiwa.

i) Sadfa ya Amani kumwona DJ akipita barabarani wakati anatafuta mtu wa kumtuma kwake Imani.
ii) Wakati Majisifu anatoroka Wangwani ndipo hapo timu ya Songoa FC inaelekea huko kwa mechi ya marudiano.

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479

iii) Ni sadfa kuwa Amani anapokuwa akitafuta kazi kwa Mtemi ndipo mchungaji wa Mtemi anaugua.
iv) Imani kusikia matangazo ya mpira akiwa katika seli na kuweza kupata habari za kakake Chwechwe Makweche.
v) Mtemi anawasili wakati Amani yumo chumbani na mkewe na kufikiria ni wapenzi.
vi) Kukutana kwa Amani na Imani kando ya Ziwa Mawewa.
vii) Amani kumnusuru Mtemi na Lowela kisadfa wanapotekwa na Gaddafi na kundi lake.
viii) Siku ambayo Amani anaandamana na Majisifu kwenda hospitalini ndiyo Amani alipewa ruhusa kurudi nyumbani.
ix) Kuanza kuugua kwa kitoto Uhuru kunatokea wakati wa mkesha wa sikukuu ya Wazalendo.
x) Imani kusahau barua ya Amani mezani na Majisifu kuipata na kujua siri ya mswada imegunduliwa. n.k.

***zozote 5 × 2 = 10***

**3.a) Taharuki - hamu ya kutaka kujua jambo litakalofuata**

i) Nasaba Bora anapotokomea asijulikane alikokuwa, kuna taharuki amekwenda wapi.
ii) Majina ya wahusika yanazua taharauki, mfano Majisifu anasifiwa na nani na kwa nini?
iii) Kutoweka kwa Bob Dj - Je, alienda wapi?
iv) Je, uhuru wa kweli, umepatikana baada ya mapinduzi au hali itakuwa ile ile?
v) Anwani inazua taharuki - *Kidagaa Kimemwozea* nani, kivipi na kwa nini?
vi) Imani kunywa maji ya Mto Kiberenge uliopigwa marufuku, je, yatamdhuru?
vii) Amani kupigwa liwato na Mtemi kisha akajikuta hospitalini, nani aliyemwauni?
viii) Baada ya Majisifu kushindwa kutoa mhadhara, kuna taharuki, je, angeweza kutoa mhadhara bora siku iliyofuata? n.k.

***zozote 5 × 2 = 10***

**4.a)i)** a) Msemaji ni Waridi
b) Msemewa ni Siki
c) Katika afisi ya Siki
d) Baada ya binamu ya Waridi kuaga na mazingira duni ya kufanyia kazi.

***4 × 1 = 4***

**b)**

i) Kuna ukosefu wa dawa
ii) Kuna njaa.
iii) Ukosefu wa vifaa vya kufanyia kazi k.m glavu.
iv) Ukosefu wa maji
v) Umaskini - kula uporo
vi) Ukosefu wa ajira.
vii) Ubadhirifu
viii) Unyakuzi wa mali ya umma - ardhi
ix) Wizi - fimbo ya Meya
x) Mishahara duni
xi) Askari kuwapiga waandamanaji
xii) Mfumo wa tenga-tawala.
xiii) Vitisho n.k.

***zozote 8 × 2 = 16***

**5.a)**

i) Msemaji ni Meya
ii) Wasemewa ni: Bili, Diwani I na Diwani II
iii) Ofisini mwa Meya
iv) Walikuwa wanapanga namna ya kuuza fimbo ya Meya

***4 × 1 = 4***

**b)**

i) Meya
ii) Ni mbadhirifu
iii) Ni dikteta
iv) Ni mfisadi
v) Ni mbinafsi
vi) Ni mlafi
vii) Ni kiongozi
viii) Ni mkali
ix) Ni msaliti
x) Ni mjinga
xi) Ni mwongo
xii) Ni mwoga n.k.

***za kwanza 4 × 2 = 8***

**5.c)**

i) DIWANI III
ii) Ni kielelezo cha viongozi waadilifu
iii) Ni kielelezo cha watetezi wa haki
iv) Ni kiwakilishi cha viongozi wazalendo
v) Kupitia kwake tunaona uongozi wa Meya wa tenga-tawala.
vi) Ni kielelezo cha viongozi wenye msimamo thabiti
vii) Kupitia kwake tunaona uwajibikaji wa daktari Siki.
viii) Kupitia kwake tunafahamu umuhimu wa kuwa na mlahaka mwema.
**ix)** Kupitia kwake tunafahamu hali ya uchumi wa Cheneo. n.k.

***Zozote 4 × 2 = 8***

**6.**

i) Msemaji ni kananda
ii) Msemewa ni Mwatela
iii) Nyumbani kwa Mwatela
iv) Kananda alikuwa ameambulia ujauzito na alitaka kuoelewa na Mwatela.

***4 × 1 = 4***

**b)**

i) Msemewa ni Mwatela
ii) Ni mwenye vitisho
iii) Ni katili
iv) Ni mdanganyifu

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479

v) Ni mlevi
vi) Ni tajiri
vii) Ni mwenye bidii
viii) Ni mwenye majuto
ix) Ni mzinzi.
***za kwanza 4 × 2 = 8***

**c)**
i) Anapigwa
ii) Dhuluma za kimapenzi
iii) Ajira wakiwa wadogo
iv) Wanadanganywa
v) Kunyang'anywa watoto
vi) Wanauzwa kama watumwa.
vii) Wanapata vitisho kutoka kwa wanaume
viii) Wanawake kuwa na wanaume wazinzi
ix) Hawana usemi mbele ya wanaume n.k
***Zozote 4 × 2 = 8***

**7. Tamaa**
i) Lucy alikuwa akiota miaka mingi kwenda London kwa sababu ni nchi ambayo imeendelea sana. Km barabara pana zilizojaa magari n.k.
ii) Alitamani muluki ya haraka haraka.
iii) Uingereza wakimbizi walipewa nyumba au makazi, na starehe nyinginezo
iv) Lucy alipitapita jijini macho yake yakitazama nyuso za wazungu - vijana na wazee
v) Lucy kumkimbilia mzee mmoja wa kizungu mkofu, mbovu.
vi) Katika ukumbi wa sinema, Lucy hakuona mchezo akifikiria wakati utakapoisha apate zawadi aliyoahidiwa.
vii) Lucy anatamani kuomba zawadi kubwa ya kuchukuliwa Uingereza.
viii) Lucy anatamani Crusoe afe.
ix) Alitaka ifike kesho kutwa akarithishwe ile mali.

**Mauti**
i) Lucy kuolewa na mwanamume mzee asiye na nguvu za aina yoyote.
ii) Kumtunza mzee mkongwe - kumkanda, kumlisha n.k.
iii) Anaanza kuchoka kuishi na mzee ambaye hawezi kumchangamsha kwa namna yoyote.
iv) Lile jumba lilimzidishia hali ya upweke.
v) Lucy alianza kumchukia Crusoe
vi) Awali Lucy alipuuza masomo na hakufaulu vizuri.
vii) Lucy alipata ajali ya gari na kupoteza uhai wake.
***Mwanafunzi agusie pande zote.***
***Tamaa 6 × 2 = 12***
***Mauti 4 × 2 = 8***

**FASIHI SIMULIZI**

**8.a)**
i) Huburudisha.
ii) Hukuza lugha.
iii) Hutambulisha jamii
iv) Hufikirisha
v) Huhifadhi historia ya jamii
vi) Hukuza ubunifu
vii) Hushauri na hufunza maadili
viii) Huleta mahusiano bora katika jamii tofauti.
ix) Huendeleza amali za jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
x) Huwasaidia wanajamii kuielewa historia yao.
xi) Huhifadhi kitamaduni wa jamii na kuuendeleza n.k.
***Kutaja ½***
***Kueleza ½***
***Zozote 5 × 1 = 5***

**b)**
i) Ukosefu wa pesa za kugharamia utafiti.
ii) Kushukiwa na wanajamii
iii) Ukosefu wa vifaa na ujuzi wa kuvitumia
iv) Ukosefu wa usalama.
v) Matatizo ya usafiri kutokana na miundo msingi.
vi) Matatizo ya hali ya anga.
vii) Kutokuwa na muda wa kutosha wa utafiti.
viii) Wanaohojiwa wanaweza kudai malipo.
ix) Kikwazo cha lugha.
x) Kuharibika kwa vifaa vya kufanyia utafiti.
xi) Mielekeo hasi kuhusu utafiti wa fasihi simulizi .
xii) Vizingiti vya kidini. n.k.
***za kwanza 5 × 1 = 5***

**c)**
i) **Rara nafsi** - Huu ni ushairi wa kinafsi ambao hutungwa na mtu kuelezea hisia, matatizo na fikra zake mwenyewe.
ii) **Hotuba** - Ni maelezo au taarifa ambayo hutolewa mbele ya hadhira kuhusu mada fulani.
iii) **Miviga** - Ni sherehe za kitamaduni ambazo kufanywa katika kipindi maalum cha wakati.
iv) **Ulumbi** - Huu ni uwezo na ustadi wa kuzungumza kwa ufasaha.
v) **Ngomezi** - Ni fasihi ya ngoma na ala zingine za kimuziki bila kutumia maneno.
***5 × 2 = 10***

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479